# AckySHINE.com

# Kuumbwa kwa mtu, Mungu alivyoumba binadamu

By DIN - Melkisedeck Leon Shine · August 2, 2015

Mafundisho ya Msingi ya Kanisa Katoliki: Makala za Katoliki · #Karibu AckySHINE · #Katoliki: Uumbaji

Mtu ni kiumbe pekee chenye mwili na roho kilichoumbwa kwa sura na mfano wa Mungu. Mungu alipotaka kumuumba mtu alisema "Tumfanye mtu kwa mfano wetu na sura yetu" (Mwa. 1:26-27)

Kuumbwa kwa sura na mfano wa Mungu maana yake tuna roho zenye akili na utashi yaani uwezo wa kutofaitisha mema na mabaya na zitakazoishi milele.

Watu wa kwanza walikua ni Adamu na Eva(Hawa), ambapo Adamu aliumbwa kwa udongo na kupuliziwa roho yenye uhai, na Eva aliumbwa kwa mfupa wa ubavu wa Adamu, akamtia roho (Mwa 2:7 na Mwa 2:21-24)

Baada ya kuumba watu Mungu aliwafundisha Dini, ambapo Dini ni mabo yatupasayo kutenda kwa Mungu Bwana wetu na Baba yetuMungu ametuumba ili tumjue, tumpende, tumtumikie tulipo wazima hapa duniani hata mwisho tukishakufa tuende kwake Mbinguni katika makao ya raha milele (Mwa. 2:7; Mt 19:17; Yoh 14:1-3 na Yoh 17:24).

Mungu aliwapa watu wa kwanza neema ya utakaso na neema nyingine nyingi na kukaa paradisi wenye heri bila kufa (Mwa 2:16-17), Lakini Adamu na Eva walitenda dhambi ya kutotii, wakataka kuwa kama Mungu lakini bila Mungu na pasipo kufuata maagizo ya Mungu.(Mwa 3:1-16)

Dhambi ya asili na kosa la Adamu na Eva

Adamu na Eva walitenda dhambi ya asili ambayo ni hali ya kukosa utakatifu na hali ya asili ya urafiki na Mungu ambayo kila binadamu anazaliwa nayo.

Baada ya kutenda dhambi yao ya kiburi na uasi walipewa adhabu zifuatazo;

Baada ya kosa la Adamu Mungu aliahidi kuwaletea Mkombozi. (Mwa 3;15)